

*“Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali; ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo.”*

1 Petro 1:6-7

Wapendwa Marafiki,

Kwa miezi michache iliyopita nimekuwa nikitafakari ni nini maana ya kuwa na imani halisi. Wanawake wengi wa kizazi kipya katika makanisa yetu na sehemu za kazi za Kikristo hutafuta kujihusisha na wanawake ambao wako wazi na wanaujua ukweli wa Biblia kwa ajili ya maisha yao wenyewe. Wanawatafuta wanawake ambao wako tayari kushuhudia majaribu ya maisha yao halisi na kujifunza pamoja katika jamii namna ya kupata matumaini ya kuvumilia wakati wa majaribu.

Ni muhimu sana leo hii kufunua imani halisi kwa sababu kuna hofu nyingi na wasiwasi kuhusu wakati ujao. Kwetu sote, miaka miwili iliyopita ilijawa na changamoto ambazo sio halisi kuhusu mabadiliko. Hali hii imeacha wengi wetu tukiwa waoga kusonga mbele katika ulimwengu huu ambao kwa sasa sio wa kawaida tena. Hatuwezi kamwe kurudi katika enzi za “wakati uliopita,” lakini Tunawezaje kuyajua yale ambayo ndio “ya kawaida” kwa ajili ya leo? Tunalipata wapi tumaini letu?

Ninaamini kwamba tumaini letu la kuishi leo na wakati ujao lipo kwa Yesu pekee. Kama tumempokea Yesu na kumwamini kama Mwokozi wetu, Biblia inasema kwamba tutapokea urithi wa uzima wa milele pamoja na Mungu milele (1 Petro 1:3-4). Upendo wa Mungu ulikuwa mkuu kiasi kwamba Mungu alimtumia Yesu afe kwa ajili ya dhambi zetu ili tuishi milele pamoja naye. Mungu anatamani kuwa na mahusiano na sisi na kutoa vipawa vyema kwa ajili ya watoto wake.

Kwa miezi ya Julai na Agosti, tunaomba kwa ajili ya huduma yetu huko Asia. Ni maombi yangu kwanza kwamba ujue urithi wako katika Yesu kisha ndipo tuombe kwa ajili ya wanawake wetu walioko Asia kwamba nao waweze kuujua urithi wao katika Yesu. Tafadhali omba kwamba wanawake watembee katika amani kamilifu ya Mungu wakijua kuwa siku moja wao nao watapokea urithi wa uzima wa milele.

---

*Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu; tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu. and decay. 1 Petro 1:3-4*

---

Ili kupata mawazo zaidi kwa ajili ya tafakari yako juu ya imani halisi, tafadhali soma makala yangu, “*Kutafuta Matumaini Leo*” katika toleo hili.

Katika Yeye mioyo yetu ifurahi.



Dkt. Peggy Banks // Mkurugenzi Ulimwenguni // Wanawake Wenye Tumaini wa TWR